

## WASIMAMIZI MSIWE KIKWAZO KUKWAMISHA ZOEZI LA UCHAGUZI

Mkuu wa Wilaya ya Ileje Mh.Farida Mgomi ametoa rai kwa wasimamizi wasaidizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji, Wilayani hapa, kutokuwa kikwazo cha kukwamisha zoezi la Uchaguzi,pale watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao wakati wa Uchaguzi.

Mhe .Mgomi ametoa rai hiyo wakati akifungua semina ya mafunzo ya Wasimamizi Wasaidizi ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji iliyofanyika katika ukumbi wa RM wilayani hapa, ambapo amewahimiza wasimamizi hao wa uchaguzi kuwa daraja litakalowaunganisha wananchi kufanya maamuzi ya kuchagua kiongozi bora atayeleta maendeleo na kuimarisha Amani na utulivu katika vijiji na vitongoji vyao.

Aidha Mhe Mgomi amewasisitiza wasimamizi kuzingatia umakini wakati watakapokuwa wanatekeleza majukumu ya uchaguzi ili kuondoa uwepo wa migogoro itakayotokana na uzembe na hivyo amewahimiza wasimamizi hao kuzingatia uwazi, haki na uzalendo wakati wa zoezi la uchaguzi, sambamba na kufuata miongozo,kanuni na taratibu za Serikali katika zoezi La Uchaguzi.

Sambamba na hayo wasimamizi wa uchaguzi wamehimizwa kuimarisha mahusiano na wadau mbalimbali wa uchaguzi ili kuweka urahisi wa suala la hamasa kwa wananchi kujitokeza kuijandikisha na kupiga kura ili kumpata kiongozi bora.